



**Na Rais
Henry B. Eyring**
Mshauri wa Pili katika
Urais wa Kwanza

Shiriki Kitu UNACHOAMINI

Baba yangu alikuwa mwanasayansi. Wakati mmoja nilisoma hotuba ambayo aliitoa kwa kikundi kikubwa cha watu. Ndani yake, aliongelea juu ya Uumbaji na Muumba kama alivyozungumza kuhusu sayansi. Nilijua kuwa wachache katika kikundi kile walishiriki imani yake. Hivyo kwa mshangao nilimwambia, “Baba, ulitoa ushuhuda wako.”

Aliniangalia, akiwa na mshangao usoni pake na kusema, “Nimefanya hivyo?” Hakuwa hata amejua kuwa amekuwa jasiri. Alikuwa amesema kitu alichojua kuwa ni cha kweli.

Sisi sote ambao tumebatizwa tumeahidi kushiriki injili. Tunaweza kusali kwa imani ili tuweze kuhisi upendo wa Mwokozi kwa ajili yetu na kwa ajili ya wote tunaokutana nao. Utafurahia kuhusu Kanisa la Bwana na kazi Yake, na itajionyesha. Kusema kile unachoamini itakuwa ni sehemu ya wewe ulivyo. ●

Imechukuliwa kutoka “A Child and a Disciple,” Liahona, Mei 2003, 29–32.

Njia Rahisi za Kushiriki


Unaweza kushiriki injili katika njia nyingi. Andika kitu ambacho ungesema kwa kila mtu ili kushiriki kitu anachoamini. Kitu cha kwanza kimefanywa kwa ajili yako.

Wikiendi yako ilikuwaje?



Vizuri!
Nilienda
kanisani.

Watu wengi wana imani tofauti za kidini. Je, wewe unaamini nini?



Papi wangu ni mgonjwa. Je, wewe utasali kwa ajili yake?



VIELELEZO NA ALYSSA TALLENT